



TAARIFA KWA UMMΑ

KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA AWAMU YA PILI MAUNGANISHO YA HUDUMA YA MAJISAFI

5.9.2024

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (**DAWASA**) inawatangazia Wananchi wa Mikoa ya **Dar es salaam na Pwani** waliokamilisha taratibu zote za kupata huduma ya majisafi kutoka **DAWASA** kuwa, Mamlaka imeanza zoezi la utoaji wa vifaa kwa ajili ya maunganisho mapya ya huduma ya majisafi.

Zoezi hili litaenda sambamba na kutoa **control number (kumbukumbu namba ya malipo)** kwa Wananchi waliokamilisha taratibu za awali, yaani Survey (upimaji) katika maeneo yao.

Hatua hii inafanyika baada ya kukamilika kwa mafanikio makubwa kwa awamu ya kwanza ya zoezi hili ambapo **Wananchi takribani 3,497 waliunganishiwa** huduma ya majisafi hadi kufikia Julai 2024.

Mamlaka inasisitiza Wananchi kuwasiliana na kufika ofisi za kihuduma **DAWASA** ili kupata huduma.

Imetolewa na

Kitengo cha Mawasiliano - DAWASA

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kituo cha huduma kwa wateja
0800110064 (Bure) au 0735 202 121 (WhatsApp tu)